


**“Ewe Mwana wa Roho! Shauri langu la kwanza ni hili: Uwe na moyo safi, mwema na
ung’ao . . .”**




“Kanyageni njia ya haki, kwakuwa hii, kwa hakika, ndiyo njia iliyonyooka”



**“Ewe Rafiki! Katika bustani ya moyo wako usipande chochote
ila waridi la upendo . . .”**



“Ukweli ndiyo msingi wa njema zote za binadamu.”




**“Kutoa na kuwa mkarimu ni sifa Zangu;
heri ni yake yule ajipambaye mwenyewe kwa njema Zangu.”**



“Amebarikiwa yule ampendeleae nduguye kabla yake yeye mwenyewe.”



**“Ewe Mwana wa Mtu! Furahia katika furaha ya moyo wako,
ili uweze kustahili kukutana Nami na kuuakisi uzuri Wangu.”**



“Tunapaswa wakati wote kudhihirisha ukweli wetu na uadilifu . . .”



**“Ewe Mwanawa Mtu! Jinyenyekeze mbele Yangu,
ili kwa hisani Nipate kukutembelea.”**



“Uwe mwenye furaha. Uwe mwenye shukrani. Inuka kutoa shukrani kwa Mungu, kwamba utoaji shukrani wako uweze kupelekea kwenye ongezeko la majaaliwa.”



**“... acha urembo wako uwe msamaha na rehema na kile kinacho
furahisha mioyo ya wapendwa wa Mungu.”**



“Rembesheni ndimi zenu, Enyi watu, kwa ukweli, na pambeni roho zenu kwa pambo la uaminifu.”



**“Ufalme wa Mungu umeanzishwa juu ya usawa na haki,
na pia juu ya rehema, huruma, na wema kwa kila roho iliyo hai.”**




“Juwa kwamba pambo lako la kweli linapatikana katika upendo wa Mungu na katika kujitenga kwako na yote ila Yeye . . .”




**“Chanzo cha utukufu wote ni kukubali chochote kile
Bwana ametujalia, na kuridhika na kile Mungu Ameamuru.”**



**“Amebarikiwa yule achanganyikae na watu wote katika
roho ya wema mkubwa kabisa na upendo.”**



**“Chanzo cha ujasiri na uwezo ni uendelezaji wa
Neno la Mungu, na uthabiti katika Upendo Wake.”**




**“Kamwe usipoteze imani yako kwa Mungu. Daima kuwa mtumainifu,
kwa fadhila za Mungu kamwe haziachi kutiririka juu ya mtu.”**



**“Uaminifu ni mlango mkuu kabisa uelekezao
kwenye utulivu na usalama wa watu.”**




**“Wakeni, Enyi watu, kwa joto la upendo wa Mungu, kwamba
ninyi muweze kuwasha mioyo ya wengine.”**




“Ewe Mwana wa Kuwa! Wewe ni taa Yangu na nuru Yangu iko ndani yako. Pata mng’ao wako kwayo na usitafute mwengine kuliko Mimi.”



**“Ni mwenye furaha yule mwaminifu ambaye amevaa vazi
la jitihada ya juu na ameinuka kuihudumia Hoja hii.”**



“Yeye, kwa kweli, ataongeza zawadi yao wale wanaostahimili kwa subira.”



**“Daraja lako litakuwa lenye ubora wa juu kabisa,
kama utaendelea kuwa thabiti katika Hoja ya Bwana wako.”**